# *Agosti*

## *Yesu aliwacha kiti chake cha enzi ili akutukuze, Nivigumu kiasi gani kwako wewe kuacha enzi zako kwa sababu yake.*

Agano jipya lina twambia kuhusu mtu aliye heshimika, ambaye hangeweza kumfuata yesu kikamilifu sababu alipenda pesa zake sana . Unaweza kujisomea habari hii mwenyewe katika Luka18. Yesu anafupisha tukio hili kwa kushiriki ilivyo vigumu kwa matajiri kupeana mamlaka ya mali zao kwa wengine, hata Mungu.

Sio pesa tu watu wanangangana ilikubaki kwenye mamlaka. Mara nyingi watu hushindwa kutoa maoni yao,kuacha kufukuzana na mambo,kukata tamaa kwa mungangano hata wanapo jikuta wakienda kinyume na neno la Mungu na mapenzi yake. Kujitolea kwa uongozi wa Yesu kuna tulazimu tumueke kwenye enzi za maisha yetu. Yesu aliwacha enzi zake kwa utukufu wako, ni vigumu kiasi gani kwako wewe kuacha enzi zako kwa sababu yake?

*Ombi la leo*

Bwana ulimtoa mwanao Yesu kwangu. Sikitu kwangu mimi kuachilia mamlaka ya maisha yangu kwako.Najua unampango kwangu.Nisaidie nijue sehemu maishani yangu ambapo bado naitaji mamlaka. Wewe tu ndio Mungu.

*Maandiko ya leo*

Marko mtakatifu 8:35-36Maana mtu anayetaka kuyaokoa maisha yake mwenyewe, atayapoteza, lakini mtu atakayepoteza maisha yake kwa ajili yangu na kwa ajili ya Habari Njema, atayaoJe, kuna faida gani mtu kuupata ulimwengu wote na kuyapoteza maisha yake?

## *Kila mtu ni mtahiniwa wa kujifunza kitu*

Haswa ni urefu gani uliomo kina cha bahari ya Pacific kwa kipimo cha nukta? Ama unaweza kuniambia ni umbali gani ulioko kati ya nyota ya kaskazini na Ulimwengu kwa Kilomita hivi? Kama huyajui mambo haya basi inamanisha hujui kila kitu, na nina kuambia kama hujui kila kitu basi wewe ni mtihaniwa wa kujifunza kitu.

Inaweza kukushitua kutambua kwamba kuna watu wengine, vijana, wengine wazee, na wengine werevu na wengine si werevu, wengine matajiri na wengine maskini, wengine wameelimika, na wengine bado, wanao jua mambo usiyojua. Usiwai kujiruhusu kua na mawazo ya juu ama kujaa kiburi na kuona huwezi jifunza kutoka kwa wengine. Jinyenyekeze, kua msikilizaji mzuri na uwathamini wengine hata kama unafikiri wewe ni mwerevu kiasi gani. Kila mtu ni mtihaniwa wa kujifunza kitu.

*Ombi la leo.*

Mungu nisaidie nishughulikie kiburi changu na kupuuza kwangu. Sitaki kua wa mawazo ya juu, ama kujuinua juu ya wengine, na niwe wa kuwatharau. Leo nachagua kutembea kwa unyenyekevu na kufungua roho yangu kujifunza kutoka kwa walimu wengi na kwa hali nyingi ninazo kumbana nazo maishani. Bwana tumia siku ya leo kunifunza kitu kipya.

*Maandiko ya leo.*

1 Timotheo 6:17Waamuru watu walio matajiri katika mambo ya maisha ya sasa, wasijivune, wasiweke tumaini lao katika mali isiyoweza kutegemewa; bali wamtegemee Mungu, ambaye kwa ukarimu hutupatia vitu vyote tuvifurahie.

1 Petero 5:6Basi, nyenyekeeni chini ya mkono wa enzi wa Mungu, ili awainue wakati ufaao.

Yakobo 4:10Nyenyekeeni mbele ya Bwana, naye atawainueni.

## *Uamuzi uliofanywa kwa hasira, ni ngumu sana uwe na faida kwa mtu yoyote*

Magereza yetu yamejaa watu walioruhusu raha ya muda kuwasukuma kwa uamuzi ambao haukuwa wa faida kwa mtu yeyote. Ndoa zimefutwa kwa sababu maneno ya upumbavu na mambo ya kuchukiza yalinenwa na uamuzi ulifanywa kwa hasira tele. Watu wamewacha kazi zao ghafula kwa kuumizwa na hasira bila kutafakari matokeo ya kudumu ya uamuzi wao.hata katika ulimwengu wa kanisa, mielekeo ambayo imetengwa kwa kiungu imeachiliwa kwa sababu ya amuzi ambazo zimefanywa kwa hasira.

Hata hivyo, hasira sio shida kila wakati. Shida ni yale tunaamua kusema ama kufanya wakati wa hasira Bibilia hutuambia tuwe na hasira na wala tusifanye dhambi. Pia hatufai kuwacha jua litue tukiwa tungali na

hasira. Uliza Mungu akusaidie ukumbane na hali zinazo kukosesha amani na usifanye uamuzi kama uko na hasira.

*Ombi la leo*

Baba, nisaidie nisiwezwe na hasira zangu leo kwa kunushawishi kurudi nyuma na kuchunguza hali ilivyo kabla ya kunena ama kufanya jambo la hasira. Najua kwamba nikiruhusu roho wangu kuelekezwa na Roho Wako, nitaleta utofauti mzuri katika kila eneo la maisha yangu.

*Maandiko ya leo*

Yakobo 1:20Mwenye hasira hawezi kutimiza matakwa ya Mungu yaliyo ya haki.

Waefeso 4:26 Kama mkikasirika, msikubali hasira yenu iwafanye mtende dhambi, na wala msikae na hasira kutwa nzima.

Muhubiri 7:9; usiharakishe kwa roho yako kuwa na hasira; maana hasira hukaa kwa kiuno cha wapumbavu.

## *Mamlaka yafaa kupeanwa tu kwa watu wanaojukumika*

Kila mtu anataka kuwagusa wengine na watu wengi hutaka kujikuta katika pahali pa mamlaka ili wafanye amuzi kulingana na mtazamo wao na waone mambo yakitendwa kwa njia yao. Ni hali ya kawaida ya mwanadamu kukuta ya kwamba mara nyingi jinsi tuwazavyo ni sawa na mtazamo wetu unafaa kujalisha. Hata hivyo, sio rahisi sana kupata watu wanaotaka kuajibika kufanya kazi, kufanya mambo yafanyike, ama kukubali makosa kwa mambo ambayo hayakufaulu. Watu wengi wanataka mamlaka lakini sio wengi wanaotaka kujukumika.

Mungu anapomtafuta mtu ambaye anaweza kuaminia mamlaka ya ufalme Wake, Yeye humtafuta mtu anayekubali jukumu za kifalme, mtu anayechukua jukumu za kibinafsi kwa kueneza na kuboresha ufalme wa Mungu kwa kuishi na kufundisha Neno la Mungu kwa Yerusalemu yao ya kimithali, Yuda, Samaria na pande zingine za dunia. Unataka kitu gani? mamlaka zaidi ama majukumu zaidi? Mamlaka yafaa kupewa watu ambao wanaweza kuaminika na majukumu.

*Ombi la leo*

Baba, nifanye wakujukumika zaidi kwa ajili ya Ufalme Wako. Nisaidie kuwa shaidi mkubwa zaidi na unipe mamlaka inayoadamana na majukumu yangu.

*Maandiko ya leo*
Mithali 29:2; wakati wenye haki wako kwa mamlaka, watu hufurahi; lakini wakati mtu muovu anapokuwa mwamuzi, watu huumia kwa uchungu.

Mathayo Mtakatifu 7:29 Hakuwa kama walimu wao wa Sheria, bali alifundisha kwa mamlaka.

Mathayo Mtakatifu 8:9; Maana, hata mimi niliye mtu chini ya mamlaka ya wengine, ninao askari chini yangu. Namwambia mmoja, \`Nenda!\` naye huenda; na mwingine, \`Njoo!\` naye huja; na mtumishi wangu, \`Fanya kitu hiki!\` naye hufanya."

## *Tunafanya tunachofanya na, twapata tupatacho kwa sababu twaamua tuamuacho*

Tunawaza tuwazavyo, hisi tunavyohisi, na tunataka tutakacho kwa anjili tunaaamini tunavyoamini. Hata hivyo, tunafanya tunachofanya, na kupata kile tupatacho kwa sababu tunachagua tunacho chagua. Kama mtu aweza kugeuza anachoamini ili kiadamane na Neno la Mungu kisha achague kunena na kutenda kama Neno linavyosema baadaye itabadilisha kile tunachoamini, tunacho hisi, tunacho taka, tutendavyo, na hatimaye kile tutapata maishani. Kwa sababu tupoamini kile Neno la Mungu linasema na tutende namna Neno linaamuru, hatimaye utapata kile Neno la Mungu linaahidi. Amua siku ya leo kwamba unaenda kuamini Neno la Mungu zaidi ya hali na mambo yote umekutana nayo maishani mwako. Zaidi ya hayo, fanya uamuzi wa kuishi maisha yako kadri ya Neno la Mungu, ukifanya uamuzi wako uambatane na mapenzi Yake. Unapofanya mambo haya, utakuta maisha yako yakibadilika kidogo kidogo hadi ufanyika mfano na dhihirisho la Ufalme wa Mungu ulimwengu huu.

*Ombi la leo*
Baba, nisaidie kukumbatia Neno Lako kama ukweli. Naomba libadilishe maisha yangu kwa yote ninayosema na kutenda. Nachagua mapenzi Yako.

*Maandiko ya leo*

Yakobo 1:22 Msijidanganye wenyewe kwa kusikiliza tu neno lake, bali litekelezeni kwa vitendo.

Yohana Mtakatifu 17:17 Waweke wakfu kwa ukweli; neno lako ni ukweli.

Matendo ya Mitume 20:32; Na sasa basi, ninawaweka ninyi chini ya ulinzi wa Mungu na ujumbe wa neema yake. Yeye anao uwezo wa kuwajenga ninyi na kuwawezesha mzipate zile baraka alizowawekea watu wake.

## ***Mungu aweza kufanya kazi ndani yako na juu yako kabla Afanye kupitia kwako***

Na je kama ungehisi kama unafaa kuwa daktari wa kupasua ubongo? Juu ya hayo, wazia kwamba umebarikiwa kwa ukweli na mbinu zinazohitajika kujaribu upasuaji huo. Je mambo haya pekee yatakufanya uhitimu kufanya kazi hiyo ambayo inahitaji maarifa na umakini? La! Nakushauri kuwa pia ungehitaji uwe na elimu, mafunzo, kazi kiasi ili upate ujuzi, na labda, baada ya muda wa kujidhihirisha kuwa una uwezo, kipawa chako chaweza kugundulika, kikubalike, na kitumika kikiwa na matokeo ya kupendeza. Ni hivyo katika kila kitengo cha kumaanisha maishani. Kipawa chetu ni kipawa tu hadi tuwe tayari kufanya mwito wetu. Mwito mikuu maishani kama ndoa, jamii, na huduma zinahitaji mafundisho yanayoendelea maishani kote. Hata ingawa Mungu anataka na anatuhitaji kutumika katika ufalme Wake, anaweza kuchagua kutenda kazi ndani yako, na juu yako kabla hatimaye afanye kazi kukupitia wewe.

<u>*Ombi la leo*</u>

Mpenzi Bwana,nipe neema kukubali mwito wangu na kukubali nyakati na majira ya maadalizi ili nihitimu kikamilifu kutimiza Umeniita kufanya.

<u>*Maandiko ya leo*</u>

Waefeso 4:11-12; Ndiye aliyewapa watu zawadi: wengine aliwajalia wawe mitume, wengine manabii, wengine wawe waeneza Habari Njema, wengine wachungaji na walimu. Alifanya hivyo apate kuwatayarisha watu wote wa Mungu kwa ajili ya kazi ya huduma ya Kikristo ili kuujenga mwili wa Kristo,

Wafilipi 2:13; Kwa maana ni Mungu anayefanya kazi ndani yako ili afanye mapenzi Yake.

## *Kuna pahali katika kupenya kwako ambapo shetani hawezi kamwe kukurejesha*

Kujaribu kubadilisha maisha yako unaweza kuonekana ni vigumu mara ya kwanza, hata ni  kama haiwezekani kwa wengine kutimiza. Kubadilika kwa maisha kunaonekana haswa ni ngumu kwa wale watu waliofungwa na _mitindo ya tabia za uzoefu._Hali ya kushangaza ni kuchukua hatua tatu mbele na mbili nyuma tena. I naonekana ya kwmba kila jaribio la urejesho linakumbana na majaribu baada ya jaribio la kushindwa, kuteleza na kurudia tabia za ka na kutenda dhambi tena. Watu wengi hufinyika katika njia ya kujaribu kubadilisha maisha na wanakata tama. Wanahisi kana kwamba hawawezi kuendelea. Wamekosea. Kuna pahali katika kupenya kwako ambapo shetani hawezi kamwe kukurejesha. Jiweke katika njia inayofaa ya urejesho kulingana na Neno la Mungu na ubaki katika njia hiyo. Hakuna shida ambayo hauwezi kuitatua, kuishinda, am kujitenga nalo kwa kufanya mapenzi ya Mungu. Ukianguka, amka, jikung’ute na ujaribu tena … utafaulu.

*Ombi la leo*

Baba, nisaidie kutambua ya kwamba kutofaulu sio kushindwa na kwamba Haujanizuia kufaulu. Mzuie shetani kunijaribu zaidi ya uwezo wangu na unisaidie kurejea kutokana na kila kua anguka katika Jina la Yesu. Amina.

*Maandiko ya leo*

Kutoka 14:13; Musa akawaambia watu, Msiogope, simameni tu, mkauone wokovu wa BWANA atakaowafanyia leo; kwa maana hao Wamisri mliowaona leo hamtawaona tena milele.

1 Wakorintho 10:13; Majaribu mliyokwisha pata ni ya kawaida kwa binadamu. Mungu ni mwaminifu, naye hataruhusu mjaribiwe kupita nguvu zenu, ila pamoja na majaribu, yeye atawapeni pia nguvu ya kustahimili na njia ya kutoka humo salama.

## *Kufaulu kwako mara nyingi hupitia kwa wengine … kwa hivyo uwe mkarimu*

Ni nachunga kanisa ambalo ni kubwa sana na limefaulu mbele ya macho ya watu wengi. Tumefunza na kuweka mamishonari, tukajenga makanisa, tukaajiri wanaochunga mayatima, tukaweka rasilmali kwa mahospitali, tukawapa vyakula sehemu za malisho, na sasa niko na wawakilishi duniani kote. Jua halitui kwa kazi ambayo inatendwa kupitia juhudi za huduma ambayo Mungu ameniamini nayo. Hata hivyo, fanaka sio zangu. Ingawa utukufu wote tunampa Mungu, hakuna jambo hata moja kati ya hizi lingefanyika kama wengine hawangeinunua maono, wajitolee kwa rasilmali zao na kuweka mikono yao kutenda kazi. Kuna watu wakuu wenye kibali kuniliko ambao wanang'ang'ana kusimamisha huduma zao na, bado, yangu inanawiri. Kwanini? Ni kwa sababu ya neema ya Mungu? Pengine katika njia zingine, lakini kwa njia nyingi zaidi ya hizi mimi huvutiwa kuelewa ya kwamba fanaka zetu mara nyingi hutegemea watu wengine wanaojitolea muda wao, talanta,na shani, kununua bidhaa zetu, ama kuimba nyimbo zetu. Kwa hivyo, kuwa mkarimu kwa wengine.

*Ombi la leo*

Mpendwa Mungu, nisaidie kutojifikiria juu zaidi kuliko vile ninavyofaa kufikiri ila nitambue ya kwamba umeniweka katika timu iliyo na wengine wengi ambao pi wanatenda kazi kwa malengo yale yale. Nifunze kuwatambua wenzangu kwenye timu na kuwa mkarimu kwa wale wanaoshikilia vitu ninavyoviamini. Amina.

*Maandiko ya leo*

Warumi 12:3; Kutokana na neema aliyonijalia Mungu, nawaambieni ninyi nyote: msijione kuwa ni kitu zaidi kuliko mnavyopaswa kuwa. Fikira zenu na ziwe na kiasi kufuatana na kipimo cha imani Mungu aliyomgawia kila mmoja.

1 Wakorintho 12:21-22; Basi, jicho haliwezi kuuambia mkono: "Sikuhitaji wewe", wala kichwa hakiwezi kuiambia miguu: "Siwahitaji ninyi." Zaidi ya hayo, inaonekana kwamba sehemu zile za mwili zinazoonekana kuwa ni dhaifu ndizo zilizo muhimu zaidi.

***Kuna uwezo zaidi katika matarajio ya usoni kuliko tuliyofanya awali.***

Yusufu alipokuwa kijana mdogo, kulingana na rekodi za kitabu cha Mwanzo,alipata kibali kwa babake na kwa hiyo alipewa vazi spesheli lenye rangi nyingi.Koti hili la rangi nyingi lilikuwa ishara ya uzuri na kibali kwa nduguze na wengine aliokutana nao.Baadaye Yusufu anajikuta akiwa mtumwa katika nchi ya kigeni.Tena,alijionyesha kuwa mwema kiasi kwamba alipandishwa cheo na kuwa msimamizi mkuu. Baada ya kupandishwa cheo,Yusufu alisingiziwa makosa na akatiwa korokoroni.Akiwa huko alishiriki katika mwanzo mpya kwa kuyaacha yaliyopita na kutenda kazi ambayo Mungu alikuwa amempa wakati huo.Punde tu Yusufu akawa mwekezaji mkuu.Inaonekana kana kwamba ingawa majaribu ya maisha ya Yusufu yalikuwa mengi, alitia bidii na kujiweka katika nafasi bora kuliko awali kwa ajili ya siku zake za usoni.Hakika, Yusufu aliishia kuwa mkuu wa nchi ya Misri.Je,Yusufu alifanikiwaje katika nyakati zote za maisha?Alielewa kwamba kuna uwezo mkubwa katika yale tunayotarajia kufanya katika siku za usoni kuliko yale tuliyofanya hapo awali.Amua kunawiri pale ulipopandwa.

*Ombi la leo*.
Baba, nakushukuru kwa yale yote uliyoniwezesha kufanya hapo awali.Hata hivyo, natazamia uwezo ulionipa leo.Nimeamua kushiriki katika siku zangu za usoni na kunawiri pale nilipopandwa.

*Maandiko ya leo*.
Yeremia 29:11; Maana nayajua mawazo ninayowawazia nyinyi, ni mawazo ya amani wala si ya mabaya, kuwapa ninyi tumaini siku zenu za mwisho.

Isaya 43:18-19; Msiyakumbuke mambo ya kwanza, wala msiyatafakari mambo ya zamani. Tazama ninatenda neon jipya; sasa litachipuka; je! hamtalijua sasa? Nitafanya njia hata jangwani na miyo ya maji nyikani.

## ***Sauti ya nafsi ni rafiki wa karibu mradi tu unaamini sawa.***

Nafsi ndiyo makao ya akili, nia na hisia.Akili ni haraka kutoa sababu na mabishano kusaidia itikadi ya kuamini ya kuamini kwa mtu. Mpango wa akili ni kutafuta mambo yatakayoambatana na imani zetu na kukubaliana na hizo imanikwaq kutoa mabishano na misukumo mingine ili kujaribu kugusia uamuzi. Hii ndio maana sauti ya nafsi ni rafiki wa karibu wakati tunaamini kilicho sawa. Hata hivyo, wakati tunapoamini kisicho sawa, nafsi itaendelea kukubaliana na makosa yetu kwa kujaribu kutulinda kutoka nje ya kile tunachoamini. Tunawazia yale tunayowazia, tunahisi kile tunahisi, na kutaka tunataka kwa sababu tunaamini kile tunachoamini. Kwa sababu hii ni muhimu

tusitumainie sababu zetu wenyewe, mtazamo wetu, ama hisia zinazoenenda kinyume na neon la mungu. Jitazame mwenyewe kwa neno la mungu badala ya kukalimani mapenzi ya mungu kulingana na vile unavyohisi.

*Ombi la leo.*
Ewe Baba, nisaidie kutofautisha sauti zinazonizungumzia na nisikubali kila hisia kama mapenzi yako.Naamua kuchunguza mawazo na matendo yangu kwa neno lako.Nifunze ninachopaswa kuamini.

*Maandiko ya leo.*
Methali 3:5-8; Mtumaini bwana kwa moyo wako wote wala usizitegemee akili zako mwenyewe. Katika njia zako zote mkiri yeye naye atayanyosha mapito yako. Usiwe mwenye hekima machoni pako, mche bwana ukajiepushe na uovu. Itakuwa afya mwilini pako, na mafuta mifupani mwako.

## ***Jukumu la muhimu. (Asili ya kifaransa,"Noblesse oblige")***

Katika lugha ya kifaransa, noblesse oblige inamaanisha haswa "jukumu la muhimu." Hutumika mara nyingi kukubaliana kwamba mali, mamlaka na kiwango fulani cha maisha huambatana na majukumu. Una damu ya kifalme ndani ya mishipa yako. Wewe ni mmiliki katika enzi za mungu na mshiriki wa umiliki na yesu kristo. Umechaguliwa na mungu kuongoza na kutawala maishani kama wafalme na makuhani mbele za mungu. Pamoja na hili jukumu muhimu la maisha, ambapo umezaliwa mara ya pili, kunatukia jukumu fulani. Sasa unawajibika kwa uendelezaji na upanuzi wa ufalme uliomiliki…inuka na ukumbane na changamoto!

*Ombi la leo.*
Baba, nakushukuru kwa kunijumulisha katika familia yako ya kifalme. Nifunze kuelewa majukumu yangu na unipe neema ya kuyatenda kwa ukamilifu.

*Maandiko ya leo*
1 Petro 2:9; Lakini ninyi ni ukoo mteule, makuhani wa Mfalme, taifa takatifu; watu wake Mungu mwenyewe, mlioteuliwa kutangaza matendo makuu ya Mungu aliyewaiteni kutoka gizani akawaingizeni katika mwanga wake mkuu.

Wagalatia 4:7
Basi, wewe si mtumwa tena, bali mwana. Na ikiwa ni mwana, basi, wewe utapokea yote Mungu aliyowawekea watoto wake.

Ufunuo 5:10
Wewe umewafanya wawe ufalme wa makuhani wamtumikie Mungu wetu nao watatawala duniani."

## *Almasi si kitu ila tu ni kaa zee lililotengenezwa vizuri chini ya msukumo.*

Bibilia inatueleza kwamba mateso yetu ya sasa ni misukumo ya muda tu ambayo mungu anaweza sababisha kututendea kazi bali si kinyume nasi. hata mioto ya adui inaweza kutumiwa na mungu kututakasa, kutuivisha vizuri, na kutuleta katika kiwango chetu cha kuyeyuka. Katika nyakati hizi za moto wa msukumo mkuu, tunakuwa wanaoweza kufinyangwa katika mikono ya mungu na wakati majira ya moto na msukumo mkuu yamekwisha, sisi hubaki tukiwa katika mfano wa mungu, tukiwa safi na wa dhamana kuu kuliko hapo awali. Unapokumbana na maadui na misukumo ya maisha, usiwaruhusu wakusukume mpaka ukose tumaini. Lakini tambua ya kwamba almasi si kitu ila tu ni kaa zee lililotengenezwa vizuri chini ya msukumo. Endelea kusonga mbele kupitia kila majira maishani, mbali na changamoto. Vumilia magumu na misukumo ya maisha kama mwanajeshi mzuri, na umruhusu mungu ketegea fursa kutenda miujiza maishani mwako.

*Ombi la leo.*
Ewe bwana,nisaidie kuweka mtazamo wangu katika mwisho wa kitu badala ya kupitia hali mbaya ya maisha. Umba uweza mkuu na unifanye kuwa na dhamana kufanya mapenzi yako.

*Maandiko ya leo.*
2 Wakorintho 4:17-18
Taabu tunayopata ni kidogo, tena ya muda tu: lakini itatupatia utukufu upitao matazamio yote, utukufu ambao hauna mwisho.Hivyo tunatazamia kwa makini si vitu vinavyoonekana, bali visivyoonekana. Maana vinavyoonekana ni vya muda tu; lakini vile visivyoonekana ni vya milele.

Ayubu 23:10
Lakini yeye aijua njia niendayo, akisha kunijaribu, nitatoka kama dhahabu.

## *Shetani mara nyingi hukuzungumzia,kupitia wewe mwenyewe.*

Kuna sauti nyingi zinazotuzungumzia zikitupa maoni na ubishi kwa minajili ya kutusaidia kufanya uamuzi unaofaa kiini cha sauti hiyo. Sauti moja yaweza kuwa ngumu kuitambua wakati mwingine,ni sauti ya mshindani wetu , shetani. Mtume Petro amhimiza mkristo kuwa macho na kukesha kwa vile mshitaki wake ibilisi, kama simba angurumaye, huzungukazunguka akitafuta mtu ammeze.mpinge yeye ukiwa dhabiti katika imani. Mara kwa mara ,vita vikali ni vile vya akili, fikira zinazobishana moja kwa nyingine,zikizungumza nasi kupitia tuliyoyapitia ,sababu, ufuatilizi, hisia na matakwa. Mara nyingi shetani anajivaa sauti ya kweli inayokujia katika fikira zako. Jifunze kutambua sauti ya adui na kuikataa.

*Ombi la leo*
Ewe bwana nifunze kutofautisha baina ya sauti yako na ya adui. Niwezeshe kushinda.

*Maandiko ya leo.*
Yohana 10: 3-5
Mngoja mlango wa zizi humfungulia, na kondoo husikia sauti yake, naye huwaita kondoo wake kila mmoja kwa jina lake na kuwaongoza nje. Akisha watoa nje huwatangulia mbele nao kondoo humfuata, kwani wanaijua sauti yake. Kondoo hao hawawezi kumfuata mgeni, bali watamkimbia kwa sababu hawaijui sauti yake."

Yohana 10:27
Kondoo wangu huisikia sauti yangu; mimi nawajua, nao hunifuata.

## ***Mapenzi ya mungu kwa maisha yako ndio uwezo wako mkuu.***

Mto hauwezi kuinuka juu kupita chanzo chake, vivyo hivyo mtu hawezi kufanya jambo lolote jema kuliko kutimiza mapenzi ya mungu kwa maisha yake.haijalishi mtu huyu ana vipawa au talanta za aina gani, aliyoyafanya awali au lengo lake,uwezo wake hautawahi kushinda njia ambayo mungu amewatengea maishani.
Amua leo kufuata mapenzi ya mungu maishani mwako na usikubali lingine.usikubali kuchanganyikiwa au kuwa mtu ambaye ulimwengu utamwona kama mkuu ilhali umepungukiwa katika kuutimiza mpango halisi wa mungu katika maisha yako.ombi lako kila siku na liwe, ‘si mapenzi yangu, bali yako, na yatimie.’

*Ombi la leo*
Unifundishe kuyatenda mapenzi yako,kwa maana ndiwe mungu wangu;roho wako mwema aniongoze kwenye nchi sawa.(zaburi 143:10)

*Maandiko ya leo.*
Matendo 13:22
Baada ya kumwondoa Saulo, Mungu alimteua Daudi kuwa mfalme wao. Mungu alionyesha kibali chake kwake akisema: `Nimemwona Daudi mtoto wa Yese; ni mtu anayepatana na moyo wangu; mtu ambaye atatimiza yale yote ninayotaka kuyatenda.`

Waebrania 10:7
Hapo nikasema: `Niko hapa ee Mungu, tayari kufanya mapenzi yako kama ilivyoandikwa juu yangu katika kitabu cha Sheria."`

Zaburi 40:8
Kufanya mapenzi yako, ee mungu wangu, ndiyo furaha yangu. Naam, sheria yako imo moyoni mwangu.

## ***Unaposhiriki injili, kumbuka ndiyo habari njema.***

tunaelezwa kuwa watu wengine huona bilauri ikiwa nusu kujaa au nusu bila chochote.kuna pande mbili za kukubali na kukataa katika kila kipengele cha maisha. kibahati,kila mmoja hupata nafasi ya kuchagua njia inayoelekea ukweli na kuamua jinsi tutakavyoshiriki ukweli na wengine.je,ushawahi kukutana na mtu ambaye anaonekana kana kwamba ana roho ya kuhukumu?wao huwatia watu changamoto kutokana na mtazamombaya, katika jaribio la kutowafanya kutenda maovu. wakati huo huo,wengine wenye roho zilizojaa neema huwatia watu moyo kutenda mema katika mtazamo bora kuwashawishi kutenda yaliyo sawa. Unaposhiriki injili kwa watu wengine kumbuka nene ‘injili’ linamaanisha habari njema.pengine waweza kupata ufanisi zaidi kwa kumueleza mtu uzuri wa kumwishia mungu badala ya kumueleza yatakayotendeka wasipomwishia mungu.

*Ombi la leo.*
Ewe bwana,nijaze neema na rehema,ufafanuzi na msamaha,matarajio na kusaidia zile nafsi ninazokutana nazo. Na nishiriki habari njema nao wote badala ya habari mbaya. Nisaidie kuwaelekeza mbinguni,si kuzimu. Amina

*Maandiko ya leo.*

Warumi 2:1-4
Basi, rafiki, kama unawahukumu wengine, huwezi kamwe kujitetea haidhuru wewe ni nani. Kwa maana, kwa kuwahukumu wengine, unajilaani wewe mwenyewe kwa vile nawe unayafanya mambo yaleyale unayohukumu. Tunajua kwamba hukumu ya Mungu kwa wale wanaofanya mambo kama hayo ni hukumu ya haki. Lakini wewe, rafiki, unayewahukumu wale wanaofanya mambo kama hayo bali wewe pia unayafanya, je unadhani utaiepa hukumu ya Mungu? Au labda unaudharau wema wake mkuu, uvumilivu wake na saburi yake, bila kutambua kwamba wema wake huo una shabaha ya kukuongoza upate kutubu?

## ***Siku za usoni zitanena ukweli.***

Bibilia ina madai mengi kuhusu ufalme wa mungu na siku zetu za usoni. Madai mengine huwa mazuri sana kiasi kwamba hatuamini. Kwa mfano, 'mkikaa ndani yangu, na mapenzi yangu ndani yenu,mkiomba lolote nitawapa.'haijalishi ukuu wa ahadi za mungu,zote zinapatikana kupitia njia moja tu….imani yetu. Siku moja sote tutasimama mbele ya mungu na macho yetu yatafunguliwa ili tuelewe neno lake ni kweli na tulikuwa na uwezo wa kupata yale aliyotuahidi katika neno lake kama tu tungemwamini na kutenda kazi katika imani. Siku za usoni zitanena ukweli. Hata hivyo,ukweli waweza kutendeshwa kazi leo kwa imani yako.amini neno la bwana. usiwe wa mwisho kuliamini.

*Ombi la leo.*
Mungu,naamua kudhamini neno lako kama mamlaka makuu na ya mwisho katika mambo ya maisha. Nakiri kwamba neno lako ni la kweli na nitayaishi maisha yangu kwa imani.

*Maandiko ya leo.*
Yohana 15:7
Mkikaa ndani yangu na maneno yangu yakikaa ndani yenu, basi, ombeni chochote mtakacho nanyi mtapewa.

Yohana 14:12-13
Barnaba akaitwa Zeu, na Paulo, kwa vile yeye ndiye aliyekuwa anaongea, akaitwa Herme. Naye kuhani wa hekalu la Zeu lililokuwa nje ya mji akaleta fahali na shada za maua mbele ya mlango mkuu wa mji, na pamoja na ule umati wa watu akataka kuwatambikia mitume.

Marko 11:22-24
Yesu akawaambia, "Mwaminini Mungu. Nawaambieni kweli, mtu akiuambia mlima huu: `Ng`oka ukajitose baharini` bila kuona shaka

moyoni mwake, ila akaamini kwamba mambo yote anayosema yanafanyika, atafanyiwa jambo hilo. Kwa hiyo nawaambieni, mnaposali na kuomba kitu, aminini kwamba mmekipokea, nanyi mtapewa.

## ***Upendo wa kweli ni wa wale walio tayari kuhatarisha mioyo yao kwa siku za usoni.***

Mungu alikupenda sana hata akamtoa mwanawe wa pekee ili kununua uwezekano wa wewe kempenda.mungu hakutoa mwana wake wa ziada ila mwana wake wa pekee nayo bibilia yatueleza kuwa kristo alitufia tulipokuwa wenye dhambi.haya yote yalifanywa bila hakikisho kuwa yeyote atatambua ,jivunia au kukubali toleo la kuwa katika familia ya mungu.huo ni upendo wa kweli. Mungu alionyesha upendo wake kwetu alipohatarisha moyo wake kwa matarajio ya usoni na wewe.usiuvunje moyo wa mungu.mpende kwa sababu alikupenda kwanza na usiogope kumuiga mungu.upendo wa kipekee waweza pia kukutaka uhatarishe moyo wako kwa wengine kwanza kabla waonyeshe upendo wao kwako.

*Ombi la leo*.
Nataka kukushukuru bwana kwa kunipenda na kunipa mwana wako aniokoe kutokana na dhambi zangu na kununua uhuru wangu. Nakupende milele,ninataka kuwa karibu nawe na zaidi kuwa kama wewe katika yote nifanyayo.nipe neema ya kuwapenda wengine kwa upendo wa roho wako wa kweli.

*Maandiko ya leo*
1 Yohana 4:7-8
Wapenzi wangu, tupendane, maana upendo hutoka kwa Mungu. Kila mtu aliye na upendo ni mtoto wa Mungu, na anamjua Mungu. Mtu asiye na upendo hamjui Mungu, maana Mungu ni upendo.

Warumi 5:8
Lakini Mungu amethibitisha kwamba anatupenda, maana wakati tulipokuwa bado wenye dhambi, Kristo alikufa kwa ajili yetu.

1 Yohana 4:19
Sisi tuna upendo kwa sababu Mungu alitupenda kwanza.

## ***Yako ya jana yakiwa makubwa kiasi kwamba yanaweka kivuli kwa yako ya kesho,yako ya usoni yanafunikwa na yaliyopita.***

Maamuzi unayofanya kila siku maishani mwako hutengeneza tarajio la jinsi utakavyoamua kuendesha maisha yako katika siku za usoni. Mpangilio wa maisha tunayojitengenezea kwa mawazo,maneno na matendo huonyesha watu wengine sisi ni nani na huwapa matarajio ya haki ya siku zetu za usoni. Kwa hiyo ni muhimu tuchunguze mpangilio wetu wa maisha ili tusifanye makosa yale yale zaidi ya mara moja. Lazima tufahamu wakati tumejiwekea sauti isiyo sawa na kujiwekea picha tusiyotaka kujulikana kwayo. Watu wengine hukujua, hukushtumu na kuweka matarajio kwako kulingana na jinsi walivyokuchunguza katika maamuzi ya maisha. Yako ya jana yakiwa makubwa kiasi kwamba yanaweka kivuli kwa yako ya kesho, basi yako ya usoni yanafunikwa na yaliyopita na Hakuna anayetarajia mabadiliko kutoka kwako…. Washangaze! Amini nikwambiapo kuwa kile wenzako wanafikiria juu yako huleta utofauti. Si shida yao tu, yaweza kuwa yako haraka sana.

*Ombi la leo.*

Ewe bwana sitaki kujulikana kama mtu mvivu, asiyetegemewa, mkali, mchunguzi,mchoyo,au asiyejali. Bali,natamani kujulikana kwa uzuri ili wengine waone upendo wako, uaminifu na neema yako maishani mwangu. Nisaidie kujichunguza na nibadilike ninapostahili ili wengine wamtarajie Yesu kutoka kwangu.

*Maandiko ya leo*.

Mithali 22:1
Heri kuchunga jina jema kuliko mali nyingi, na neema kuliko fedha na dhahabu.

1 Wakorintho 11:31
Kama tungejichunguza wenyewe vizuri hatungeadhibiwa hivyo.

## ***Kujiunga kunajalisha: kikundi unachojiunga nacho kitaathiri hatima yako.***

Vikundi mara kwa mara hutafuta watu wapya na kuchukua viongozi wapya. Awali, nimeona watu wazuri na waliomaanisha vyema walio na tamanio la kuleta mabadiliko wakikubali kujiunga na au uongozi katika vikundi bila kuelewa malengo ya vikundi hivyo. Makundi haya hupatikana makanisani,kazini na sehemu zingine za jamii. Vingine vina

malengo yenye mazao ilhali vingine havina mwelekeo. Hivyo ndivyo ilivyokuwa wakati wa musa alipowaongoza wana wa Israeli kutoka misri ,kupitia jangwani hadi nchi ya ahadi.njiani,musa alikumbana na vikundi vitatu vinavyotambulika ambavyo bado vinatafuta watu hadi leo. Kulikuwa na kikundi cha 'twende ng'mbo ile' (yoshua na kaleb), kikundi cha 'tunyakueni' (korah dathani na abiramu), kikundi cha 'nimeshapitia' (wapelelezi kumi) na kikundi cha 'imekwisha' (kizazi cha wanaisraeli waliofariki jangwani.). kabla ya kujiunga na kikundi chochote au kukubali kueneza maono yao, hakikisha kikundi kina kiongozi anayefaa na kinakubaliana na maono ya kiongozi wake.

*Ombi la leo.*

Ewe mungu,nisaidie nisipande maovu au kujitungia uongo,au kuwa sehemu ya tendo la ukaidi dhidi ya viongozi wanaofaa na amri ya ufuatilizi uliyoweka kanisani mwangu,kazini au jamii. Nipe neema ya kupambanua ninayotaka kufanya na yale ya siri ya wanaotaka kunihusisha katika maovu. Nataka kuwa zaidi kama wewe.

*Maandiko ya leo.*

Hesabu 14:28-30

Waambieni kama nishivyo asema bwana, hakika yangu kama ninyi mlionena masikioni mwangu ndivyo nitakavyowafanyia ninyi. Mizogz yenu itaanguka katika jangwa hili na wote waliohesabiwa miongoni mwenu kama jumla ya hesabu yenu, tangu waliopata umri wa miaka ishirirni na zaidi, hao walioninung'unikia hakika yangu hamtaingia ninyi katika nchi ambayo niliinua mkono wangu ya kwamba nitawaketisha humo isipokuwa kalebu mwana wa yefune na yoshua mwana wa nuni.

## *Usihatarishe mwondoko wa mungu ili kuwapendeza watu.*

Ukweli mara nyingi haudhihirishwi kwa kuinua mikono na tunapojaribu kumfurahisha kila mtu huwa tunaishia kutomfurahisha yeyote. ni kwa sababu hii neno la mungu lina mpangilio wa kiungu wa uchaguzi kwa nafasi za umuhimu wa kimsingi. Mungu ndiye amuinuaye mmoja katika nafasi ya uongozi na kumshusha mwingine. Hakika, mtume Paulo anasema katika kitabu cha warumi 13,ya kuwa Hakuna mamlaka kupita mamlaka ambayo yanaruhusiwa na mungu. Kama mungu ameamua kuwazungumzia watu kupitia watu wengine, basi sisi twawezaje kuuacha mwelekeo ambao mungu amewapa viongozi wake? Hata hivyo, watu wengi hawasemi ukweli kuhusu maadili ya mungu ili kuwafurahisha watu na kuwafanya wahisi kuwa wana sehemu. Usiuache mwito wa mungu ili kuwapendeza watu. Kuwa jasiri, mwenye

nguvu, mkarimu, lakini uwe imara na mungu anaponena,usitupilie mbali kuwafurahisha watu.

*Ombi la leo.*
Baba, nipe nguvu, ushujaa na kujitolea ili kuamua kutotingizika katika neno lako au kujaribu kuwafanya viongozi wangu kutonena ukweli kulingana na neno lako ili kunipendeza mimi au wengine. Nisaidie kuwa mkarimu lakini pia mwenye kutaka kuyatimiza mapenzi yako.

*Maandiko ya leo.*
Wagalatia 1:10
Sasa nataka kibali cha nani: cha binadamu, ama cha Mungu? Au je, nataka kuwapendeza watu? Kama ningefanya hivyo, mimi singekuwa kamwe mtumishi wa Kristo.

Wagalatia 1:15,16
Lakini Mungu, kwa neema yake, alikuwa ameniteua hata kabla sijazaliwa, akaniita nimtumikieMara tu alipoamua kunifunulia Mwanae kusudi niihubiri Habari Njema yake kwa watu wa mataifa mengine, bila kutafuta maoni ya binadamu,

.Matendo 13:22

Baada ya kumwondoa Saulo, Mungu alimteua Daudi kuwa mfalme wao. Mungu alionyesha kibali chake kwake akisema: `Nimemwona Daudi mtoto wa Yese; ni mtu anayepatana na moyo wangu; mtu ambaye atatimiza yale yote ninayotaka kuyatenda.`

## *“Hakuna giza” haitafanya kazi.*
Funzo la kwanza ambalo mungu anatufunza kumhusu yeye linapatikana katika Mwanzo 1. anasema kwamba aliumba mbingu na nchi, na alipofika mahali fulani akaona alichokuwa ameumba hakikukubalika. Nchi ilikuwa ukiwa,tena tupu,na giza lilikuwa juu ya uso wa vilindi vya maji. Katika hali ya kuchukua alichokuwa nacho na kukifanya kuwa alichotaka, kwanza alifikiria mwelekeo wake kisha akasema, “iwe nuru!” na ikawa. Mungu anatufunza kuwa kuna nguvu katika kukiri sawa hasa tunapopata tunapopata mpango na kuusema kwa imani. Tambua kwamba mungu hakukana kwamba hakukuwa na shida, wala hakuilaani shida hiyo au kuilalamikia. “Hakuna giza!” kamwe haingetenda kazi hapa. Ukikumbana na kitu maishani mwako ambacho hakikubaliki usikane kwamba kipo,lakini kataa kuendelea kwake kwa kuchukua hatua zifaazo. Kuwa kama mungu: tafuta mpango na uanze kunena unachotaka kwa jicho la imani yako na itakuwa hivyo.

*Ombi la leo.*
Baba wa mbinguni, nifunze njia zako na unipe hekima ya kupanga maisha yangu kulingana na mapenzi yako ili kutabiri siku za usoni kwa ndoto iliyo moyoni mwangu.

*Maandiko ya leo.*
Marko11:22-24
Yesu akawaambia, "Mwaminini Mungu. Nawaambieni kweli, mtu akiuambia mlima huu: `Ng`oka ukajitose baharini` bila kuona shaka moyoni mwake, ila akaamini kwamba mambo yote anayosema yanafanyika, atafanyiwa jambo hilo. Kwa hiyo nawaambieni, mnaposali na kuomba kitu, aminini kwamba mmekipokea, nanyi mtapewa.

Mithali 18:20-21
Tumbo la mtu litajazwa na matunda ya kinywa chake, atashiba mazao ya midomo yake, mauti na uzima huwa katika uwezo wa ulimi, na wao waupendao watakula matunda yake.

Waebrania 6:12
Msiwe wavivu, bali muwe kama wale wanaoamini na wenye uvumilivu na hivyo wanapokea yake aliyoahidi Mungu.

## ***Moyo ulio mgumu hautaruhusu neno la uponyaji liguse panapoumia.***

Watu wanapoumia, mara kwa mara hufanyika wagumu na wanaruhusu uchungu huo kuifanya mioyo yao kuwa migumu na isiyopenyeka. Machungu haya yasipohudumiwa hayaponi na yanaishia kuwa na uchungu zaidi. Hata hivyo, kwa kila uchungu wa mwanadamu, mungu ana neno la uponyaji. Neno lake ni kama dawa ya uponyaji mradi tu lifike panapo maumivu.wewe tu ndiye unayeweza kuvunja nafasi ya moyo wako isiyotumika na kuruhusu neno la mungu la uponyaji kugusa panapoumia. Labda mungu anamtuma mmoja wa watumishi wake neno au wimbo kwa ajili yako, likibeba neno lake la uponyaji kukutana na hitaji lako. Usiache ugumu wa roho yako uzuie neno la uponyaji kugusa panapoumia.

*Ombi la leo.*
Ewe bwana, nachagua leo kufungua roho yangu kwa neno lako hata katika sehemu nilizoumizwa. Sitajikinga na kukosa mazuri yako maishani mwangu. Wacha neno lako la uponyaji liguse ninapoumia na kufanya upya maisha yangu.

*Maandiko ya leo.*
Marko 16:14
Mwishowe, Yesu aliwatokea wanafunzi kumi na mmoja walipokuwa pamoja mezani. Akawakemea sana kwa sababu ya kutoamini kwao na ukaidi wao, maana hawakuwaamini wale waliokuwa wamemwona baada ya kufufuka.

Hosea 10:12
Jipandieni katika haki, vuneni kwa ufadhili, uchimbueni udongo wa mashamba yenu, kwa maana wakati umewadia wa kumtafuta bwana hata atakapokuja na kuwanyeshea haki.

## *Isiyochunguzwa na isiyojaribiwa mara nyingi huwa isiyobadilika; chunguza, jaribu,badilisha!*

Njia moja nzuri ya sisi kuendelea kubadilisha panapohitaji mabadiliko ni sisi kujitia changamoto na kuweka malengo ya kubadilisha mawazo yetu na/au tabia yetu na kuweka maisha yetu sawa na neno la mungu. Hata hivyo, mara nyingi hatujitii changamoto kubadilika kwa sababu hatujui sehemu tunazohitaji kubadilisha. Kwa sababu hii bibilia inatuhimiza tujichunguze na tujionee kama tunaishi kulingana na imani. Tukijichunguza na kujihukumu vilivyo, bibilia inasema hatutahukumiwa. Mara nyingi, maisha yasiyochunguzwa hubaki bila changamoto hivyo basi kubaki vile vile. Jichunguze…jitie changamoto…. Na jibadilishe kuishi kulingana na neno na mapenzi ya mungu.

*Ombi la leo.*
Ewe bwana,nena nami unionyeshe ninapofaa kubadilika. Nitajitia changamoto katika sehemu hizo kuwa na tabia njema maishani na kuwa zaidi kama wewe.

*Maandiko ya leo.*
2 wakorintho 13:5
Mwenye upendo hakosi adabu, hatafuti faida yake binafsi, wala hana wepesi wa hasira; haweki kumbukumbu ya mabaya,

1 wakorintho 11:31
Kama tungejichunguza wenyewe vizuri hatungeadhibiwa hivyo.

2 wakorintho 3:18
Basi, sisi sote ambao nyuso zetu hazikufunikwa, twaonyesha kama katika kioo, utukufu wa Bwana; tunabadilishwa tufanane zaidi na huo

mfano wake kwa utukufu mwingi zaidi. Hiyo ni kazi yake Roho wa Bwana.

## *Ukweli u tayari kuwa wa uchungu iwezekanavyo ili ubaki ukweli.*

Sisi sote tumejaribiwa kudanganya pale ukweli ulipomaanisha kumkosea rafiki. Lakini hata kama tungebadilisha ukweli ili kuufanya mwepesi, basi si ukweli tena. Wazia kujenga nyumba bila kutumia vipimo vya viwango vya kweli. Ukiongeza inchi hapa na kupunguza kipimo cha mraba pale matokeo ya mwisho yanaweza kuwa na uharibifu. Wakati mwingine ukweli ni mgumu kukubali naye yesu alifahamu haya vyema kuliko mwingine yeyote. Ilhali,aliwaambia rafiki zake kuacha tamaa zao za uchoyo ili kumfuata yeye. Haukuwa ujumbe wa kukubaliwa lakini wenye nguvu. Ukweli tu ndio ulio na uwezo wa kuokoa maisha ya mwanadamu. Chochote chini ya hiyo ni bure. Unaweza kutakaswa kwa ukweli… neno la mungu ni kweli.

*Ombi la leo.*
Bwana, hata ikiwa ukweli unaumiza, nisaidie kusikia na kuwa tayari kubadilika. Pia nipe neema ya kuwa msema kweli kwa wengine ili wafaidike kwa ukweli.

*Maandiko ya leo.*
Yohana 17:17
Waweke wakfu kwa ukweli; neno lako ni ukweli.

Marko 8:34 ; Kisha akauita umati wa watu pamoja na wanafunzi wake, akawaambia, "Mtu yeyote akitaka kuwa mfuasi wangu, lazima ajikane mwenyewe, auchukue msalaba wake, anifuate.

Yohana 8:32; Mtaujua ukweli, nao ukweli utawapeni uhuru."

## *Katika agano la kale, Mungu alipotaka kazi kutendwa, mwana alizaliwa. Katika agano jipya, mungu alipotaka kazi kutendwa, kanisa lilizaliwa.*

Kupitia agano la kale, mapenzi na kazi za mungu zilitimilika kupitia watu binafsi waliozaliwa kwa wakati unaofaa na makusudi. Hawa wanaume na wanawake wa mungu waliwakilisha sauti ya mungu kwa ulimwengu uliopotea na watu wanaougua ambao hawangesikia kutoka kwa mungu mwenyewe.kwa hiyo kila wakati kazi ilipotaka kufanywa

mtoto alizaliwa. Hivyo ndivyo ilivyokuwa na musa, samsoni, na esta na yesu.
Agano la kale limeangazia miaka elfu nne ya historia kupitia vizazi tofauti, na kusudi moja… kucukua maumbile ya mungu kutoka shamba la edeni mpaka kwa mesaya.agano jipya linaangazia kizazi kimoja katika muda wa huduma. Makusudi yake ni kumwandaa kila muumini kufikia ulimwengu wao na injili ya yesu kristo kwa kila kizazi. Hii inatendeka kupitia huduma ya kanisa. Katika agano la kale, mungu alipotaka kazi itendeke,mtoto alizaliwa. Katika agano jipya,mungu alipotaka kazi itendeke,kanisa lilizaliwa. Husika kanisani.

*Ombi la leo.*
Baba, naliombea kanisa langu na nafasi yangu katika kazi yako ya ufalme. Niweke katika mwili wa waumini kama inavyokupendeza na uniunganishe pamoja na wengine kutumikia mausia yako katika kizazi hiki. Amina.

*Maandiko ya leo.*

Waefeso 4:11-16; Ndiye aliyewapa watu zawadi: wengine aliwajalia wawe mitume, wengine manabii, wengine wawe waeneza Habari Njema, wengine wachungaji na walimu. Alifanya hivyo apate kuwatayarisha watu wote wa Mungu kwa ajili ya kazi ya huduma ya Kikristo ili kuujenga mwili wa Kristo, na hivyo sote tuufikie umoja wa imani na kumjua Mwana wa Mungu; tuwe watu waliokomaa na kuufikia utimilifu wake Kristo mwenyewe. Basi, hatutakuwa tena kama watoto, tukitupwa na kupeperushwa huko na huko kwa kila upepo wa mafundisho wanayozua watu wadanganyifu, ili wawapotoshe wengine kwa hila. Ila, sisi tukisema ukweli kwa moyo wa mapendo tutakua zidi katika kila jambo kulingana na Kristo ambaye ndiye kichwa; chini ya uongozi wake, viungo vyote vya mwili hushikamana pamoja, na mwili wote hutegemezwa kwa msaada wa viungo vyake. Basi, kila kiungo kikitekeleza kazi yake ipasavyo, mwili wote hukua na kujijenga katika upendo.

## *Kutofanya uamuzi mara nyingi ni kuamua kutofanya lolote*

Mara kwa mara maishani, tunakumbana na shida ambazo mara nyingi hatutaki kukabiliana nazo. Katika majira haya, mara nyingi tunaamua kutofanya lolote, kuahirisha tukitumai kwamba shida zitajisuluhisha au zipotee. Mara nyingi hii si kweli. Mambo mabaya yakiachwa hayawi mazuri, bali huharibika kushinda awali. Mungu hutuhitaji kushiriki

katika kutafuta suluhu. Hata hivyo, kuna habari njema! Twaweza kukutana na milima yoyote kwa imani kwamba Mungu yu nasi, si kinyume nasi. Ana jibu kwa kila shida tunayopitia na yuko tayari kujiunga nasi kama tu tutawaendea na kukumbana na maadui wetu. Mara nyingi, shida ngumu tunazopitia huwa tu ni uamuzi wa kufanywa, na ni wewe tu unayeweza kufanya lolote kuhusu haya.

*Ombi la leo*

Baba, nisaidie leo kukumbana na kila hali kwa maombi na imani ya kwamba unajua jawabu na utaniongoza katika ufanisi. Nakupa hofu zangu.

*Maandiko ya leo*

Mithali 1:5; Mwenye hekima asikie na kuongezewa elimu, na mwenye ufahamu ayafikie mashauri yenye njia.

1 Wafalme 18:21; Naye Eliya akawakaribia watu wote, akanena, 'mtasitasita katikati ya mawazo mawili hata lini? Bwana akiwa ndiye Mungu, mfuateni; bali ikiwa Baali ni Mungu, haya! Mfuateni yeye.' Wale watu hawakumjibu neno.

Yoshua 24:15; Nanyi kama mkiona ni vibaya kumtumikia Bwana, chagueni hivi leo mtakayemtumikia; kwamba ni miungu ile ambayo baba zenu walitumikia ng'ambo ya mto, au kwamba ni miungu ya wale Waamori ambao mnakaa katika nchi yao; lakini mimi na nyumba yangu tutamtumikia Bwana.

## ***Kama ni sugu yaweza kuwa ya kipepo***

Je, umewahi kuwa na shida ambayo haindoki, shida ambayo, haijalishi ulichofanya, na bado hupati suluhu? Mtume Paulo alikuwa na shida kama hiyo katika 2 Wakorintho12. Aliuita mwiba katika mwili, mjumbe wa shetani aliyetumwa kumpiga. Neno 'kupiga' hapa lamaanisha, gonga kitu mara kadhaa.. Kila wakati mtume Paulo alipohisi alikuwa na ushindi, adui angerudi na kumgonga tena. Ilikuwa ya kuchosha sana hadi mtume Paulo akamlilia Mungu amsaidie. Jibu alilopewa na Mungu linatupa tumaini hadi leo. Mungu alimwambia mtume Paulo kuwa neema yake ilikuwa imemtosha. Ukijipata katika shida ambayo haibanduki, yaweza kuwa na mizizi yake katika ulimwengu wa kipepo, mjumbe wa shetani aliyetumwa kwa kuvunja moyo ili kukufanya ukate tamaa na kukubali kushindwa. Usishindwe! Mlilie Mungu na utapata kuwa neema yake yakutosha wewe pia.

*Ombi la leo*

Ewe Bwana, ninaomba ya kwamba uniondolee majaribu yote, misukumo, na shida maishani mwangu ambayo yanatamani kusababisha kushindwa kwangu. Hata hivyo, yale unayosababisha kwa majira ya mapenzi yako, ninaomba unipe neema ya kuvumilia na katika unyonge wangu nipate nguvu zako, katika Jina la Yesu, Amina.

*Maandiko ya leo*

2 Wakorintho 12:7-10; Lakini, kusudi mambo haya makuu niliyofunuliwa yasinifanye nilewe majivuno, nilipewa maumivu mwilini kama mwiba, mjumbe wa Shetani mwenye kunipiga nisijivune kupita kiasi. Nilimsihi Bwana mara tatu kuhusu jambo hili ili linitoke. Lakini akaniambia: "Neema yangu inatosha kwa ajili yako; maana uwezo wangu hukamilishwa zaidi katika udhaifu." Basi, ni radhi kabisa kujivunia udhaifu wangu ili uwezo wake Kristo ukae juu yangu. Kwa hiyo nakubali kwa radhi udhaifu, madharau, taabu, udhalimu na mateso, kwa ajili ya Kristo; maana ninapokuwa dhaifu, ndipo ninapokuwa na nguvu.

## *Safari kuu ya mwanadamu huanza na shauku*

Je, wataka nini? Ni nini shauku ya moyo wako? Watu wengi sana wanaishi, kufanya kazi na kuhudumu katika hali ambazo hawana shauku nazo. Watu wengi wanachukia kazi zao na hawaridhishwi na uhusiano wao wa kimsingi ama kutotosheka na wanayofuata maishani ilhali Mungu yu tayari kuweka shauku mioyoni mwao ya mapenzi yake, makusudi yake na mpango wake wa maisha yao. Mungu hakukusudia uishi maisha yako ukitamani kuishi tofauti. Ana mpango, kusudi, na atakupa shauku ya moyo wako. Mtafute leo; mwitie maadamu anapatikana, nawe utajifurahisha kwa Bwana, naye atakupa haja za moyo wako na ukumbuke safari kuu ya mwanadamu huanza na shauku.

*Ombi la aleo*

Baba, nakabidhi njia yangu kwako. Sababisha mawazo yangu yatiwe msingi na uweke shauku lako kwa maisha yangu katika moyo na akili yangu. Ninapojifurahisha kwako, timiza tumaini langu ili niwe na furaha maishani na ninapokutumikia.

*Maandiko ya leo*

Zaburi 37:4; Nawe utajifurahisha kwa Bwana, naye atakupa haja za moyo wako.

Marko 8:34; Kisha akauita umati wa watu pamoja na wanafunzi wake, akawaambia, "Mtu yeyote akitaka kuwa mfuasi wangu, lazima ajikane mwenyewe, auchukue msalaba wake, anifuate.

Mithali 13:12; Kilichotarajiwa kikikawia kuja, moyo huugua. Bali haja ya mtu ikipatikana ni mti wa uzima.

1 Petro 2:2; Kama vile watoto wachanga wanavyotamani maziwa, nanyi pia mnapaswa kuwa na hamu ya maziwa halisi ya kiroho, ili kwa nguvu yake mpate kukua na kukombolewa.

## ***Mungu ni Mungu wa mpangilio ... maisha yanahitaji mpango***

Mungu alipoumba mbingu na nchi na kujaza nchi kwa mimea na wanyama, alikuwa anafululiza mpangilio, mpango, kudumisha maisha, maisha ya wana wake, na ulimwengu ujao. Mungu ni Mungu wa mpango. Nyuzi za DNA sio matukio ya ghafla au kujirudia kusikofaa, maisha yako katika mpangilio wa kiungu. Maisha yanahitaji mpango, wa kuzaliwa na kuishi kikamilifu. Je, una mpango kwa maisha yako? Je, mpango wako ni mpango wa Mungu? Maisha bila mpangilio ni hatia, ni kama maisha bila mpango. Leo, Mungu yu tayari kukupa maono ya siku zako za usoni na kukuonyesha hatua inayofuata kuelekea maono hayo. Ukimwita atakuitikia, naye atakuonyesha mambo makubwa magumu usiyoyajua. Kusudia kujua mpango wa Mungu maishani mwako.

*Ombi la leo*

Ewe Mungu, naomba ulete mpangilio katika hatua zangu na unionyeshe njia nitakayotembelea na hatima nitakayochagua. Najua una mpango kwa maisha yangu. Naomba ujidhihirishe kwangu ili niichukue hatua yangu inayofuata kwa ujasiri.

*Maandiko ya leo*

Yeremia 29:11; Maana nayajua mawazo ninayowawazia ninyi, asema Bwana, ni mawazo ya amani wala si ya mabaya, kuwapa ninyi tumaini siku zenu za mwisho.

1 Wakorintho 14:40; Lakini yote yafanyike kwa heshima na kwa utaratibu.

Zaburi 119:133; Uzilelekeze hatua zangu kwa neno lako, uovu usije ukanimiliki.

Zaburi 37:23; Hatua za mtu zaimarishwa na Bwana, naye aipenda njia yake.

## *Kuna vita vya akili, akilini*

Katika 2 Wakorintho 10 maandiko yanatuhimiza kutumia silaha zetu za vita vya kiroho ambazo zina uwezo katika Mungu, hata kuangusha ngome. Tukiendelea, tunaelekezwa mahali ambapo tutalenga silaha zetu za kiroho tukiwa vitani. Hapa, tunaambiwa tusipigane dhidi ya shetani, dhidi ya mapepo ya giza, au maadui wengine wa mioyo yetu. Lengo la silaha hizi za kiroho ni akili zetu. Mungu angelitaka tulenge mawazo yetu, msingi wa ufahamu wetu na ujuzi na vile vile maisha tunayowazia. Tunaambiwa tuweke chini kila wazo na kila kitu kinacho inuka, kijiinuacho juu ya elimu ya Mungu, na tukiteka nyara kila fikira ipate kumtii Kristo. Kuna vita vinavyoendelea na jukumu letu ni kufanyisha kazi silaha zetu za vita vya kiroho dhidi ya vile vitu ambavyo vinatoa akili zetu kwa Mungu. Jinenee … shinda vita hivi … katika uwanja mkuu wa vita vya kiroho - akili yako.

*Ombi la leo*

Ewe Bwana, itie akili yangu nguvu ya kupinga kuwaza mawazo ya adui zako. Weka chepeo cha wokovu juu yangu ili nilinde kuta za mawazo yangu, na kutowaruhusu maadui kuweka ngome. Nifunze ukweli nami nitaweka chini kila fikira. Hili ni jukumu langu. Nisaidie kulitimiza.

*Maandiko ya leo*

2 Wakorintho 10:3-5; Kweli tunaishi duniani, lakini hatupigani vita kidunia. Maana, silaha tunazotumia katika vita vyetu si silaha za kidunia, ila ni nguvu za Mungu zenye kuharibu ngome zote. Tunaharibu hoja zote za uongo, na kubomoa kila kizuizi cha majivuno kilichowekwa kuipinga elimu ya Mungu; tunaziteka fikira zote na kuzifanya zimtii Kristo.

Warumi 12:1-2; Kwa hiyo, ndugu zangu, maadam Mungu ni mwenye huruma nyingi, nawasihi kwa moyo wote: jitoleeni nafsi zenu kwa Mungu kama tambiko iliyo hai, takatifu na yenye kupendeza. Hii ndiyo njia yenu halisi ya kumwabudu. Msiige mitindo ya ulimwengu huu, bali Mungu afanye mabadiliko ndani yenu kwa kuzigeuza fikira zenu. Hapo ndipo mtakapoweza kuyajua mapenzi ya Mungu, kutambua jambo lililo jema, linalompendeza na kamilifu.

## ***Kushinda nafsi kutaongeza kwenye ufalme, ilhali kufanya wanafunzi kutajumulisha ufalme***

Kuna utofauti wa kueleweka katika msemo wa kale, “mpe mtu samaki na utakuwa umemlisha kwa siku moja, mfunze mtu kuvua samaki na utakuwa umemlisha maisha yake yote.” Ni sawa na ukweli tunaouona katika tofauti kati ya kanuni za kuongeza na kujumulisha. Tukiongeza nambari mbili pamoja, jawabu hilo ni chini sana ya jawabu ambalo tungepata kama tungejumulisha nambari hizo. Huenda ikawa hii ni sababu moja ya Mungu kuwaelekeza waumini kwenda ulimwenguni kote na kufanya wanafunzi. Mara tu mwanafunzi anapofanywa, ataendelea kuzaa matunda peke yake kwa kufanya wanafunzi wengine; hivyo basi ufalme utaendelea kuongezeka kwa njia kuu na kuwa na uhakika wa siku za usoni. Kila muumini anatakiwa kuwa mshindi wa nafsi, lakini kushinda nafsi ni mwanzo tu. Tuna jukumu la kufunza kila mkristo mchanga jinsi ya kuwa mshinda nafsi. Jitolee kwa mwito mkuu na uhusike katika mpango wa Mungu wa kuupanua ufalme. Fanya wanafunzi huku ukiwafunza kufanyia wengine jinsi ulivyowafanyia.

*Ombi la leo*

Baba, na niendelee kuwa mwenye hekima na kushinda nafsi kwa ajili ya ufalme wako. Hata hivyo, Bwana, nitie moyo ili nisiwache msukumo wangu ukome papo. Nipe neema ya kuwafunza wanafunzi watakaoendeleza kazi ya ufalme wako katika kizazi chao hadi Yesu atakaporudi.

*Maandiko ya leo.*

Mithali11:30; Mazao ya mwenye haki ni mti wa uzima; na mwenye hekima huvuta roho za watu

2 Timotheo 2:2; Chukua yale mafundisho uliyonisikia nikitangaza mbele ya mashahidi wengi, uyakabidhi kwa watu wanaoaminika, ambao wataweza kuwafundisha wengine pia.

Mathayo 28:19-20; Nendeni basi, mkawafanye watu wa mataifa yote wawe wanafunzi wangu; mkiwabatiza kwa jina la Baba, na la Mwana, na la Roho Mtakatifu. Wafundisheni kushika maagizo yote niliyowapeni. Nami nipo pamoja nanyi siku zote; naam, mpaka mwisho wa nyakati."